# MLIMA WA HABARI NA MVUMO WA INJILI



JAMES KALEKWA

# MLIMA WA HABARI NA MVUMO WA INJILI.

MLIMA WA HABARI NA MVUMO WA INJILI

JAMES KALEKWA

# Orodha ya Yaliyomo

Ulewa wa Ujumla ........................................................... 4

Kumiliki mlima wa habari:................................................ 7

a) Ujumbe............................................................... 7

b) Namna ya kusambaza ujumbe ............................. 10

c) Umbali wa Ujumbe ........................................... 11

Mlima huu ndiyo ni ufunguo wa kuingia mwisho:................ 12

Kundi maalum la wapiga mbiu:......................................... 14

Maarifa na Mkakati:......................................................... 16

Baa chini ya jua ............................................................... 18

Kuhusu Mwandishi:.......................................................... 19

Kuhusu New Vine Church:................................................ 20

Mawasiliano na Mwandishi: ............................................. 20

# Ulewa wa Ujumla

**Kisa mkasa:**

Kwenye eneo moja linalotoa huduma ya kuosha magari, jijini Dodoma, vijana watatu wanabishana na kuzidiana hoja kuhusu maswala ya kisiasa na kijamii (socio-political). Kijana wa kwanza anaelezea jambo, na kujenga hoja kwa ujasiri na sauti ya juu. Anavyosimulia ni kama alikuwepo vile kwenye eno la tukio; kisha kijana namba mbili kwa hisia na kukosa ustahimivu anamjibu yule wa kwanza kuwa amekosea kabisa na hana lolote analolijua. Akaanza kujenga hoja yake naye kwa muono tofauti kuhusiana na jambo hilo hilo. Pakawa na kelele nyingi kwasababu kijana wa kwanza na wa tatu hawakubaliani naye. Halafu kijana wa tatu naye akaingilia mjadala lakini hakubaliani na wenzake waliotangulia.

Baada ya majadiliano marefu ambayo yanaonekana hayatakuwa na mwisho au hitimisho la pamoja. Wakageuka na kuanza kulaumina wao kwa wao ya kwamba “Tatizo lako wewe ni mbishi”… mwingine anamwambia mwenzake “Tatizo lako wewe ni shule, hujasoma lakini unaongea sana.” Kisha yule mwingine akasema “Labda tumuulize brother hapa atusaidie…” na huyo brother ni mimi – Mchungaji!

Badala ya kuwapa majibu majibu, niliamua kuwauliza maswali ya kuwafikirisha. Kwanza nilitaka kusikia kila mmoja amefahamu vipi/amefahamia wapi taarifa hiyo? Pili, nikataka kusikia kila mmoja ana taarifa kiasi gani kuhusiana na jambo hilo.

Mmoja aliona kipande kifupi cha video kilichobandikwa kwenye mtandao wa Youtube na watu fulani; mwingine aliona mjadala wa kwenye moja ya mitadao wa kijamii. Kuna mtu aliweka post na wengine wakaja kuchangia na kutoa maoni; na mwingine aliona habari iliyobandikwa na chombo fulani cha habari.

Wote hawakuona taarifa husika kwa ukubwa wake.

Kutokea hapo nilihitimisha ya kwamba vyombo vya habari vina nguvu ya kuiathiri jamii wa upana sana. Kuna vijana wako wanabishana kwa sababu ya jambo ambalo hawana undani wake lakini wameona kwenye vyombo vya habari; kuna watu wanapaza sauti juu, wanakashifiana, wako tayari kumwaga jasho lao kutetea hoja fulani na/au kushambulia hoja fulani kwa kuwa tu kuna jambo wapata kwenye vyombo vya habari.

Kwao, ilimradi kimetokea kwenye vyombo vya habari, ni kweli!

Hawawezi kutofautisha maoni, uchambuzi, msimamo na taarifa. Wao wanakula kama inavyoachiliwa. Ni huzuni na kweli.

Iwe unajua ama haujui, mlima wa habari unahusika kutengeneza "ukweli wa jamii" husika. Hapa jamii huundwa!

**Mambo ya kufahamu:**

- Kwenye mlima huu kuna maswala ya upashanaji wa habari.
- Lengo ni kusababisha agenda zijulikane/zifahamike na zisikike kwa nguvu
- Mlima huu umekusudiwa kuwafikishia watu wengi taarifa kwa muda mfupi na/au muda mwafaka kwa kadiri inavyowezekana.
- Mlima huu umeenda mbali zaidi. Si tu kwamba unatoa habari, bali unatengeneza habari kwa kuamua nini ni habari na nini si habari.
- Ni kwa njia hii baada ya muda jamii hufinyangwa na kuwa ya uelekeo fulani.

Kwa kitabu hiki ningependa kutambulisha nia ya Mungu ya kutaka habari zake, agenda yake ya Kristo tumaili la ulimwengu na muundo wa maisha ndani ya Kristo tukiwa hapa duniani vifahamike na kufanyika msaada kwa watu.

Kanisa limeaminiwa kubeba ajenda ya Mungu; Mwamini umekusudiwa kusababisha habari za Kristo Yesu zinasikika kwa nguvu na kufanyika msaada kwenye maisha ya watu.

Hebu tusome neno la Kristo linasemaje kisha nikutambulishe kwenye mambo kadhaa.

"**Piga kelele**, **usiache, paza sauti yako kama tarumbeta**; Uwahubiri watu wangu kosa lao, Na nyumba ya Yakobo dhambi zao." Isaya 58:1

"Tena **habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote,** kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja." Mathayo 24:14 [SUV]

"Kwa maana **dunia itajazwa kwa maarifa ya utukufu wa BWANA**, kama maji yaifunikavyo bahari." Habakuki 2:14

## Kumiliki mlima wa habari:

Ili uweze kuukalia mlima wa habari, kama mwamini n aka utukufu wa Mungu, ni lazima uwe umebeba mambo yafuatayo:

### a) Ujumbe

- Mungu hatumi watu kwenda kupiga kele, kuhubiri, kutangaza kile wanachojisikia. Anawapatia ujumbe. Kwenye maandiko yaliyotangulia utaona kuna kitu kinaitwa *"Habari njema ya Ufalme";* ama utaona

*"Uwahubiri watu kosa lao"* au utaona *"maarifa ya utukufu wa Mungu"*. Mwamini asiye na ujumbe au agenda ya ufalme, atakuwa kama kopo linalopiga kelele.

- Ni vizuri kujua kwenye ufalme huu kuna UJUMBE – Ujumbe ambao hubadilisha maisha ya mtu milele. Ujumbe wetu ni Yesu Kristo; ujumbe wetu ni msalaba; ujumbe wetu ni maisha ndani ya Yesu Kristo!
- Je, una uhakika na huu ujumbe? Je, unaujua ujumbe? Unauamini ujumbe? Kama jibu ni ndiyo, basi unapaswa kuusema kwa ujasiri sana. Kutokuusema ujumbe wa ufalme ni kiashiria kwamba ama hauujui au hauna uhakika nao (hauuamini)
- Iko hivi, ujumbe unaouamini ndiyo ujumbe utakaoutangaza!
- Tuna agenda ya ufalme hivyo hatupaswi kupeperushwa na agenda za falme zingine. Kuna mawakala na wabobevu wengi kwenye maswala yanayowahusu. Na wewe bobea kwenye ujumbe tulioitiwa.
- Tuko kwenye vita ya kuhakikisha ujumbe huu unawafikia watu. Hali ukijua ujumbe tulioubeba unagusa nyanja zote za kimaisha (holistic) kutokea msalabani.

Dunia inauhitaji sana. Dunia itaokolewa kwa ujumbe huu. Pigana vita! Ukweli ni kwamba kuna vita kwenye mawimbi ya upashanaji wa habari.

Mtunzi mmoja wa tenzi aliwahi kuandika wimbo uuitwa Ni ujumbe wa Bwana (I have a message from the Lord, Hallelujah)

1. Ni ujumbe wa Bwana, Aleluya!
Wa maisha ya daima,
Amenena mwenyewe, Aleluya!
Utaishi ukitazama

2. Ni ujumbe wa wema, Aleluya!
Nawe shika rafiki yangu!
Ni habari ya habari ya raha, Aleluya!
Mwenye kuinena ni Mungu.

3. Uzima wa daima, Aleluya!
Kwake Yesu utaouona.
Ukimtazama tu, Aleluya!
Wokovu u pweke kwa Bwana.

*Tazama, ishi sasa!*
*Kutazama Yesu,*
*Amenena mwenyewe, Aleluya!*
*Utaishi ukitazama.*

## b) Namna ya kusambaza ujumbe

Kuna namna ambayo Mungu ameelekeza ujumbe wake usambazwe. Si kama tunavyotaka sisi bali kama anavyotaka Yeye.

- Kupiga kelele. Mpendwa unapaswa kuwa na fujo, kuinua sauti yako, kulazimisha usikivu. Kuna neno la kiingereza "aggressive" – ubabe na kulazimisha mambo yatokee. Ndiyo taswira ninayoipata kila nikisikia Mungu anasema*"James, piga kelele!"* Umeshawahi kuona mtoto mchanga, chini ya miezi sita akiwa anawasilisha ujumbe wake? Labda anahitaji kunyonya? Amechoka? Anahitaji kubadilishiwa mavazi? Huwa Analia… anapiga kelele! Hata ukimpuuzia, haachi. Hata ukiondoka kwenye chumba alichomo, haachi. Yaani ni lazima uje umsikilize!
- Kutokuacha (Mwendelezo). Mungu anatoa malekezo "usiache". Hakuna wakati ambao unapaswa kushusha au kupunguza sauti. Sauti ya injili inapaswa kuwa endelevu kwenye kizazi chetu. Watu wakipuuza? Watu wakiacha kusikiliza? Watu wakionekana kuendelea na mambo yao? USIACHE! Unaweza kubadilisha mbinu na mtindo wa kupiga kelele… lakini usiache!

- Paza sauti yako kama tarumbeta (Hakikisha unasikika). Umeshawahi kusikia tarumbeta kwa karibu? Kuna namna unaweza ukapuuza sauti ya tarumbeta. Mungu anataka uhakikisha unasikika. Hakikisha sauti yako inapenya kwenye masikio ya watu.

c) Umbali wa Ujumbe

- Ulimwenguni mwote
- Dunia yote
- Eneo letu la kijiografia, eneo jirani, nchi jirani, dunia yote.
- Wote waifikilie toba. Haya ndiyo matokeo ya mwisho ambayo Mungu anaykusudiwa yazalishwe na ujumbe wake.

"Basi walipokutanika, wakamwuliza, wakisema, Je! Bwana, wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli ufalme? 7. Akawaambia, Si kazi yenu kujua nyakati wala majira, Baba aliyoyaweka katika mamlaka yake mwenyewe. 8. Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika **Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.**"

Matendo ya Mitume 1:6-8

Unajua moja ya tarajio la Israeli ilikuwa ni kutolewa chini ya utawala kandamizi wa dola ya Rumi. Na walitarajia atakapokuja masihi, moja ya kazi yake ni kuwarejeshea Israeli utawala wao wenyewe (wajitawale wenyewe tena); uhuru kutoka kuwa koloni la Rumi.

Wanafunzi wa Yesu wakamkusanyikia na swali lao "Unatuachaje mzee?" Wameona amefanya mambo yote makubwa, isipokuwa jambo moja tu… Ufalme!

Na Yesu anawaonyesha mkakati wa kuuleta ufalme kwenye uhalisia (actualization). Mkakati uko hivi, mtakuwa mashahidi wangu! Hakuna namna nyingine ya kuuleta ufalme wa Mungu duniani isipokuwa kufanyika mashahidi wake. Kimsingi, ufalme wake umeshakuja. Tunahitaji kualika watu wawe raia wa ufalme wake. Hatua ya pili ni ya kijiografia – tunaanza na eneo letu la kijiografia. Kisha tunaenda eneo jirani. Kisha nchi jirani na hatimaye ulimwenguni mwote.

Kila mwamini anapaswa kuuwaza ulimwengu anapotaka "kupiga kelele".

## Mlima huu ndiyo ni ufunguo wa kuingia mwisho:

Kuna siku za mwisho na kuna siku ya mwisho – siku ya kurudi Bwana Yesu Kristo kwa mara ya pili duniani.

Kibiblia, siku za mwisho zilitabiriwa na Yoeli na kuthibitishwa kuwa zimeanza kutokea kwa kinywa cha Mtume Petro, siku ya Pentekoste.

(Yoeli 2:28/Matendo ya Mitume 2:16-17)

Na kuna siku ya mwisho, ambayo Kristo Yesu atakuja mara ya pili. Hii itatokea baada tu ya injili kuufikia ulimwengu wote; kuwafikia watu wote.

Kwa sababu tofauti tofauti, kwa nyakati tofauti za kanisa, baadhi ya waamini wamekuwa wakiomba au wakiimba Yesu arudi. Hata hivyo, kwenye neno tunapewa jawabu ya kwamba kurudi kwa Yesu kutatanguliwa na injili kuwafikia watu wote. Mungu ametuamini na anatusubiria tupaze sauti kwa nguvu injili isikike kote na watu wote wafikiwe.

"Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, **bali huvumilia kwenu**, maana hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafikilie toba." 2 Pet 3:9

"... Badala yake, **Yeye anawavumilia ninyi**..." [Neno: Maandiko Mtakatifu]

"Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote**, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja**." Mathayo 24:14 [SUV]

- Dalili za mwisho kuja ni habari za Ufalme kuhubiriwa;

- Mungu anatusubiria sisi tuende mbele kwa nguvu kusambaza habari za ufalme wake [anatuaminia sana]

## Kundi maalum la wapiga mbiu:

Ni kweli jukumu la kupiga kelele na kupaza sauti kama tarumbeta ni la kila mwamini. Kila mmoja wetu amepakwa mafuta na anatarajiwa na Mungu kutimiliza jukumu hili. Hata hivyo, kuna watu ambao wanabeba wito mahususi wa "kupiga mbiu". Neno la Kristo linasema hivi:

"BWANA akanijibu, akasema, Iandike njozi ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji."

Habakuki 2:2

"... so that even **the runner** can read it." [Complete Jewish Bible]

"... so **he may run** who reads it." [English Standard Version]

"...ili **mpiga mbiu** akimbie nao." [NENO]

Kuna watu ambao Mungu ameweka wito ndani yao kuwa wapiga mbinu. Hawa ama ni wamiliki wa vyombo vya habari, wawezeshaji wa kifedha wa injili kwenye vyombo vya habari, watendaji wa upashanaji wa habari (media practinioners), watunga sera na

wasimamizi wa mlima wa habari. Hawa wote wanaweza kuitwa wadau wa habari.

Kanisa linapaswa kuwa mstari wa mbele kushikilia ajenda ya habari kwa nguvu. Wadau wa habari watokee mlima Sayuni ili kuweza kuuokoa mlima huu.

**Ushuhuda wa kusikitisha:**

Kwa kiasi fulani, nimekuwa nikufatilia maswala ya habari kwa undani. Hususani madhara ya habari kwenye maisha, utamaduni na tabia ya watu. Wakati fulani niliona chombo kimoja cha habari chenye ushawishi kwenye jamii ya vijana na watu wa mijini. Kilifanya mwaliko wa ndugu mmoja kwenye kipindi chao maarufu sana. Huyu ndugu anafahamika kuwa ndoa ya mitala yenye furaha. Yaani, ameoa zaidi ya mwanamke mmoja. Kwenye kile kipindi aliwekeza muda na kupewa muda mwingi kufafanua dhana ya ndoa za mitala. Watangazaji na wasikilizaji waliotoa mrejesho, walifurahia sana kupokea "ufunuo" huo.

Siku moja kabla ya kipindi, walitoa tangazo. Moyoni nilisikia taa nyekundu inawaka "TAASISI YA NDOA INASHAMBULIWA"

Baada ya kipindi hicho, ukisoma kwenye mitandao ya kijamii na kufuatilia maoni ya watu wengi. Utaona ni kwa namna gani wanaume wanatamani sana kuwa kama huyu ndugu; wengine wanawalaumu wake wao kwa nini "si waelewa"; na wengine walienda mbali

kuuliza kama kweli Mungu amekusudia mwenzi mmoja. Kuna wanawake walipaza sauti ya kwamba wao wako tayari kuwa "mke wa pili" iwapo kuna mwanamume wa namna hiyo atakayejitokeza.

Miezi kadhaa baadaye, akajitokeza ndugu mmoja mwenye ndoa mfano wa ile iliyopewa "airtime"; huyu mtu hakuwa anajulikana sana. Lakini alisukuma agenda mpaka akakaribishwa studioni na kupewa sehemu ya kipindi kuzungumzia aina hiyo ya ndoa.

Athari ya hivyo vipindi viwili tu kwenye mioyo ya watu na maisha ya baadhi ya wanandoa ni kubwa. Kuna watu, kwa vipindi hivyo tu, ndoa zao ziliingia kwenye migogoro isiyoisha. Kipindi kimoja kinaweza kuacha madhara ya kudumu kwenye maisha ya watu.

Huo ni mfano mmoja tu, lakini kuna mishale mimngi sana ya moto ya yule mwovu huachiliwa kwa mawimbi ya habari na watu  wengi, hata waamini huwa hawajainua ngao ya imani ili kuizima… Huwa wako "loose" kwa sababu hawatarajii vita itakuja kwa namna hii.

## Maarifa na Mkakati:

Danieli 12:4 "Lakini Wewe, Ee Danieli, yafunge maneno haya, ukakitie muhuri kitabu, hata wakati wa mwisho; wengi wataenda mbio huku na huko, **na maarifa yataongezeka**."

- Mwisho kuna ongezeko la maarifa litatokea – maarifa ya kila namna [uvumbuzi, ugunduzi, ubunifu na ustadi]
- Maarifa si mabaya tu na kuna maarifa mema!
- Kanisa linapaswa kutumia jukwaa la maarifa mema kukuza sauti ya UJUMBE; kueneza UJUMBE!
- Hapa ndipo tunapaswa kuwa kimkakati.

Tunaishi kwenye nyakati ambazo kuna kila aina ya maarifa kwenye vidole vyetu; kuna mbinu, ujuzi na suatdi mwingi sana unaweza ukatumiwa kuhakikisha sauti zetu zilizobeba ujumbe wa ufalme zinapaa. Kuna maendeleo makubwa sana ya kiteknolojia ambayo yanaweza kutumiwa kama "mwanapunda" kumbeba na kumsafirisha Yesu na kumfikisha kwa watu anatakiwa kuwafikia.

Moja ya walimu mahiri wa theolojia hapa nchini, Dr. Zakayo Nzogere aliwahi kuweka swali kwenye ukurasa wake wa facebook. Alikuwa anajiuliza iwapo Bwana Yesu angeishi zama hizi au Mtume Paulo angekuwepo kwenye nyakati zetu, je angetumia mitandao ya kijamii? Jibu lake lilikuwa ANGEKUTUMIA SANA NA KWA NGUVU! Kwa sababu lengo la Yesu ni kuwafikia watu wengi; lengo la Paulo ni kuhakikisha anayafikia makanisa mengi aliyoyafungua na kugusa jamii kubwa. Si ajabu kwamba angekuwa na akaunti za mitandao ya kijamii.

Kwa hiyo, tunapozungumzia maswala ya habari, tunapaswa kuwaza zaidi ya mifumo mikongwe (mainstream media) kama Television, radio na magazeti; tunapaswa kuwaza mifumo ya kisasa na ya zama zetu. Kanisa, tuwafuate watu waliko na ujumbe wa Yesu kwa nguvu!

## Baa chini ya jua

“Mimi nimeona watumwa wamepanda farasi, na wakuu wakienda kwa miguu juu ya nchi kama watumwa." **Mhubiri 10:7**

Kuna jambo ambalo halipasi kuwa hivyo, huitwa baa. Na moja ya baa ni wakuu kuenda kwa miguu wakati watumwa wanaendesha farasi. Kimsingi, watu wa Mungu tunapaswa kuendesha farasi; kuukalia mlima huu; kuwa na mkono kwenye nyanja hii ya habari – kumiliki vyombo vya habari, kudhamini, kutunga sera, kuwa watendaji (practitioners), kuwa wasimamizi wa sera.

Tusiachilie adui na mawakala wake watamalaki kwenye mlima huu.

Usisahau, anayeutawala mlima huu, huitawala jamii na utamadunia wake.

Ni maombi yangu ya kwamba watainuka watu watakaosababisha mvumo mkubwa wa injili kwenye zama zetu, kizazi chetu kwa kuukalia mlima wa habari kwa jina la Yesu Kristo.

## Kuhusu Mwandishi:

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis “Tai”, Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

## Kuhusu New Vine Church:

Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

## Mawasiliano na Mwandishi:

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi n audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: James Kalekwa

Instagram: james_kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-7764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

# KUHUSU MWANDISHI



**James Kalekwa** ni amemwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma.


James Kalekwa
james_kalekwa
@MchungajiJK
+255 754 917 764